

**HOTUBA YA WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI, MHE. MUSTAFA
HAIDI MKULO (MB), KWENYE MAHAFALI YA ISHIRINI NA TATU
(23) YA CHUO CHA MIPANGO YA MAENDELEO VIJIJINI TAREHE
04 DESEMBA, 2009**

***Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Mhe. Eng. Dkt. James Alex Msekela
(Mb);***

***Mwenyekiti wa Baraza la Uongozi wa Chuo, Prof. David
Kapinga;***

Wajumbe wa Baraza la Uongozi wa Chuo;

***Ndugu Constantine Slyvinus Lifuliro, Mkuu wa Chuo cha
Mipango ya Maendeleo Vijijini;***

Viongozi wa Serikali, Taasisi na Mashirika Mbalimbali;

Waandishi wa habari,

Wafanyakazi wa Chuo;

Watunukiwa;

Wanafunzi wa Chuo;

Wageni Waalikwa;

Mabibi na Mabwana.

Ndugu Mwenyekiti,

Napenda nianze kwa kuwashukuru kwa heshima mliyonipa ya kuwa Mgeni Rasmi katika mahafali haya ya 23 ya Chuo. Napenda kuchukua nafasi hii kukupongeza wewe Mwenyekiti na wajumbe wako wote kwa kukisimamia na kukiongoza vema Chuo hiki hata kufikia mafanikio haya tunayoyaona. Hongereni sana.

Aidha, nakupongeza Mkuu wa Chuo Bwana Lifuliro na timu yako ya wafanyakazi wa Chuo cha Mipango kwa kufuata na kutekeleza kwa umakini na ufanisi mkubwa maagizo na maelekezo toka ngazi za juu. Nakuombeni muendelee na juhudi hizo. Nawapongeza wahitimu mnaotununikiwa tuzo zenu leo. Juhudi zenu ndizo zilizo wafikisha hapa. Soko liko wazi japo kuna changamoto katika ajira. Kikubwa mjiepushe na anasa ambazo zinaweza kuwasababishia maambukuzi ya UKIMWI. Kumbukeni mmesomeshwa kwa fedha za Umma, Umma huo unawasubiri mkautumikie hadi ukomo wa umri wa ajira. Ninyi ni

nguvukazi na nguzo ya taifa. Kwa wale mliotoka makazini mkatumie vyema elimu na ujuzi mlioupata ili mlete tija sehemu zenu za kazi. Kuelimika kunapimwa na uwezo wa mtu kutoa suluhu ya matatizo ya jamii na wala siyo sifa za kwenye vyeti tu.

Ndugu Mwenyekiti,

Niseme kuwa yale yote uliyoyaeleza kwenye hotuba yako na ile hotuba ya Mkuu wa Chuo nimeyasikia na kuyapokea. Kwa ujumla nakubaliana nanyi kuwa taaluma ya mipango ina umuhimu wa kipekee katika maendeleo ya Nchi hasa kwa wakati huu kwa sababu kuu ifuatayo:-

Mipango ndiyo inayotafsiri dira, dhima, sera, maazimio na matamko mbalimbali ya maendeleo ya Nchi kwa kuweka malengo yanayofikiwa na mikakati inayotekelezeka. Kupitia mipango serikali inapata fursa ya kugawanya kwa uwiano vipaumbele rasilimali za Nchi. Kwa msingi huo Nchi inakuwa na uwezo wa kupima maendeleo yake kwa urahisi.

Ndugu Mwenyekiti;

Kutokana na umuhimu wa taaluma hii ya mipango kwa maendeleo ya Nchi yetu, kwa niaba ya serikali napenda kukuhakikishia wewe Mwenyekiti na wanajumuiya wote wa Chuo cha Mipango kwamba Serikali itaendelea kukijengea uwezo Chuo kwa kadiri ya mahitaji na upatikanaji wa fedha kwa kuajiri wahadhiri, watumishi waendeshaji na kuwasomesha. Lengo ni kukiwezesha Chuo kuendelea kutoa huduma iliyo bora kwa wadau wake. Ninawapongeza kwa ubunifu wa Chuo wa kufanya mafunzo kwa vitendo katika hali halisia ambayo inayotoa suluhu ya matatizo mbalimbali yanayozikabili Halmashauri zetu nchini. Serikali itazielekeza Mamlaka za Serikali za Mitaa na Wadau wengine wote wa maendeleo kutumia fursa hii inayopatikana Chuo cha Mipango.

Kutokana na hali hiyo, Serikali itaendelea kuimarisha mikakati ya upanuzi wa Chuo katika miundombinu, vifaa na vitendea kazi kwa ujumla. Nia ya serikali ni kuona Chuo kinafanikisha mambo yote yaliyokusudiwa kulingana na malengo ya kuanzishwa kwake.

Aidha, nizidi kukupongeza Mwenyekiti na Baraza lako kwa juhudi mlizozianzisha za kuendeleza kiwanja Na. 2 kitalu B kilichopo Miyuji Kaskazini na kupata maeneo mapya yaliyo jirani na Chuo. Ninasema Serikali inaunga mkono juhudi zetu na itatimiza wajibu wake.

Mwisho, narudia tena kuwashukuru kwa kunialika katika mahafali haya. Nawatakia kila la kheri wahitimu wote, wageni waalikwa na wanajumuiya wote wa Chuo cha Mipango ya Maendeleo Vijijini.

Ahsanteni sana kwa kunisikiliza